# Kudhibiti

# migogoro



# Kwa nini usimamizi wa Darasa ni wa umuhimu?

### 1. Ina simamisha kuchoka kwa walimu

Inaondoa kuchanganyikiwa na inasaidia na kuchoka ambayo inaelekeza hadi kwa "kuishiwa kwa nguvu". Tunajuwa sisi wote kuhusu watu ambao walifikiria yakuwa ni jukumu lao kutumikia mwaka kutoka waanze kuwa na watoto wanaoenda kanisa, na hawawezi ngoja mwaka uishe ili waweze kutoroka darasani. Kukiwa na chumba kimejaa watoto ambao wanatabia mbaya, huwa hawaangalii mbele kuwa na watoto wale. Wakati wa huduma unapoisha kila wiki, wanaenda wakihisi wasiwasi na wakiwa wamekasirika. Hawataki kuongea na kuimba na kuomba na wakristo wengine baada ya kanisa, lakini wanatorekea manyumbani mwao. Pahali pana usalama na watulie.



### 2. Inakuza walimu walio na furaha

Mwalimu ambaye anatumia saa moja kwenye darasa moja nzuri huwa anahuzunika wakati muda unapo isha. Labada kulikuwa na zaidi ya kufunza, lakini muda umeisha na wazazi wanangoja watoto wao. Mwalimu anatoka chumba na tabasamu na moyo mwenye furaha kwa sababu ya kuona neon la Mungu likichukua mzizi na macho ya wanafunzi yamefunguliwa kwa ukweli mpya.

### 3. Inaguza wakati ujao

Walimu huwa wanaskia ushuhuda wa kubadilika kutoka kwa wanafunzi wao ju ya vitu mabazo walifunza muda uliopita. Wanajuwa yakuwa wanaguza siku zao za usoni, wakibadilisha maisha, na kusaidia familia kuwa nzima kwa sababu watoto wanasoma jinsi ya kuishi kama yesu.





## 4. Huwa inatangaza wizara ya watoto

Baada ya kanisa walimu hawana haraka ya kwenda nyumbani kupumzika, lakini wanataka kwambia watu wengine kuhusu kitu mtoto alisema ambacho kilifanya moyo wake uimbe. Wanataka kuungana na wazazi wa watoto na wawaambie jinsi ambavyo wamefurahi yakuwa mtoto wake alikuja leo na kile ambacho waliiongea darasani. Labda mwalimu atapee wazazi swali ambalo wanaloweza kuuliza watoto kuhusu darasa, na kupea watoto nafasi kuwaambia kina mama wao na kina baba wao kile ambacho wamesoma, ama wafanye zoezi la kukariri mstari wa bibilia na kuongeza nguvu somo

## 5. Ina tia moyo kwa watu kujitolea kwenye wizara



Wakati wengine wanaona jinsi vile walimu wanafurahia kufunza, watukuwa na nia ya kujitolea kusaidia ama kusadia mwalimu aliye likizoni. Wanaweza jitolea pia kuwa walimu. Wakati mwalimu anatoka kutoka darasa la kupendeza, lenye utulivu, furaha yao itashika wengine na watataka kuihisi pia.

## 5. Watoto wanafurahia kuja darasani

Usimamizi wa darasa husaidia watoto kuhisi wakiwa na usalama,utulivu na wakiwa wamependwa. Wanaamini yakuwa mwalimu atawalinda kutoka kitu ambacho kinaweza waumiza. Kwenye mazingira yenye utulivu na usalama, watoto huwa wanasoma zaidi. Huwa hawakimbii kwa kina mama na baba zao baada ya ibada kanisani na kustaki kila mtu na kila kitu. Wazazi walioko na wasiwasi wanaweza shuku yakuwa wanafanya kitu sahihi kwa kuruhusu watoto wao kwenda darasa badala ya kukaa kwa upande wao na kukasirishwa na ibada ya kanisa. Pia, wakati darasa ilikuwa na uzoefu mzuri, inawezekana yakuwa wataalika wengine kuhudhuria.



# Ni Funguo ipi yakuwa na Darasa nzuri,na ambalo limedhibitiwa?


## FUNGUO NI:KUEPUKA SHIDA KABLA YA ZIANZE

Sababu ile muhimu sana si vile shida zinashughulikiwa, lakini kuchukua njia njema za kuzuia na kutokuwa na shida kuanzia mwanzo. Kuepuka huwa kunapatikana kwa kuwa tayari na vifaa vyote na somo. Kuwa na darasa nzuri, mwalimu lazima apee mungu masaa mingi, nyuma matukio, sio tu saa manayo darasa ina fanyika.



## I. PANGA RATIBA

Mwalimu ule mzuri huwa ana panga ratiba kwa umakini, ikiwa imeshughulikia mapendeleo, mahitaji, na umri wa watoto. Nitaenda hadi kwa maelezo zaidi muda mfupi ujao.






## 2. MIPANGO NA KUTAYARISHA VIFAA

Kama kuna hila, vifaa vyote viko tayari na vina patikana kwa urahisi, hadi kwa macho ya watoto ili waweze kutarajia shughuli yenye raha ambayo inakuja baada ya somo lao. Kuna mfano ambao umemaliziwa ili watoto waweze kuona kile ambacho watakuwa wanatengeneza.

Kama kuna kitafunio,iko tayari kupeanwa paketi yoyote imefunguliwa. Msaidizi ana jua wajibu wake na hahitaji maelezo wakati wa darasa. Mfuko wa taka uko tayari kwa ajili ya kusafisha.

Kama kuna mchezo umepangwa, vifaa vya mchezo ziko kwenye eneo ambalo litachezewa. Mwalimu amefikiria kati ya maelezo na sheria na ako tayari kuelezea haraka sheria za kucheza mchezo.



Kwanini wazo hili ni la umuhimu ivo? Kila wakati ambao mwalimu anageuka kwa darasa kutumia muda wakiendea vifaa, wanafunzi watakuwa na nafasi ya kutengeneza shida. Kuzuia kunamaanisha yakuwa hawatawai pata nafasi hio. Mara mingi wanafunzi wanasema, “mimi sijui!” na wanakataa kuhusika kwenye tabia zisizofaa. Wakijuwa yakuwa haitafanya kazi kwa sababu mwalimu anaoana, hawatajaribu kwa sababu mwalimu atawashika wakifnaya ivo.

## 3. NAKIRI HADITHI

Mwalimu lazima ajue somo vizuri sana, na asiangalie maelezo yeyote. Wakati wa somo, mwalimu akuwe anaangalia kwenye macho ya watoto, na kurekebisha hadithi kwa sababu ya majibu. Baada yah ii nitakupee vitu za kutazama na mapendekezo ya njia za kurekebisha hadithi



## 4. Tazama wanafunzi



Kama wanafunzi wanakaa nikama wameanza kuchoka, mwalimu anafaa kuwahusisha kwenye shughuli ambayo inaongeza kuelewa kwa hadithi. Simamisha hadithi, na uulize wanafunzi kusimama na kuigiza sehemu hio ya hadithi.

Wazo lingine ni kuacha hadithi na kuuliza swali ya kile kinaweza fanyika baadae. Hii bila wao kujua inavuta akili za wanafunzi nyuma hadi kwa kuwa makini. Majibu yao yataonyesha jinsi ya vile wameelewa.

Labda mwalimu ataamua kutumia vionekazo muda huo mwingine. Mwalimu anaweza gundua yakuwa hawakufurahia kuskiza kwa muda mwingi na mara hio ingine ata fupisha hadithi, ama anasimulia wakati wanafunzi wengine wana igiiza.

Mwalimu anafaa kuwa ana jaribu kufikiria kile mwanafunzi anaweza kuwa anafikiria kwa kichwa yake. Angalia kwa ishara za kuonya yakuwa mtu anafikiria kuhusu kuvuta nywele ya mwanafuzi mwingine, na kuzuia isifanyike kwa kufanya kila mtu aiigize sehemu yake ya hadithi, (kuwa kondoo, panda farasi, chota maji toka kwa kisima na kumwaga ingine na kunywa, jifanye vile uko kipofu..) kisha panga tena vile wameketi na uendelee na hadithi, ukijuwa yakuwa shida imezuiwa na watoto walipata tu raha na walikuwa hawajui yakuwa mtu alikuwa karibu kufanya kitu mbaya.



Hii ni tahadhari ambayo inaweza fanyika na mwalimu ambaye anajuwa somo vizuri sana hadi mwalimu hafikirii kile ambacho anasema baadaye, lakini anajuwa ni nini inafuata, na anafikiria jinsi ya vile ata atahri watoto walioko kwenye chumba hicho. Lengo ni kwa kikundi na kwa nani anaskiza, na sababu kwa nini hawaskizi ama hawana nia.

## 5. Rekebisha kwa ajili ya watu wengi kuwepo.



Wakati wanafunzi wako kwa umati, shida mingi huonekana, wanafunzi wanahitaji shughuli mingi kuwaweka wakiwa makini kwa hadithi wakti wanatupa umakini kwa wanafunzi wengine kwenye maeneo mengine. Mwalimu anafaa kupanga sehemu kwenye somo ambazo zinapee wanafunzi kitu cha kuongeza na



sauti zao, kuonyesha na ishara ama na kitu kuigiza na mikono yao ama miili. Baadaye, nitakwambia jinsi ya kupanga jinsi watakavyo kaa darasani.

## 6. Pangia umri wa wanafunzi

Watoto wadogo wana umakini mdogo. Ni asili kwao kuacha kuskiza na, kuanza kufikiria kitu kingine cha kufanya wakati unapita uwezo wao wa kumakinika. Inaweza kuwa wazo la kupinga. Watasumbua mtu mwingine. Darasa lote litaangalia kile wanafanya, na watafurahia kile wanafanya. Umepoteza darasa. Na hadithi yako haiskizwi na yeyote.

Wakati unatayarisha somo, fanyia zoezi,wekea muda, na weka shuguli za mwili kwa ajili ya watoto. Usiwaulize wakae chini na waskize kwa zaidi ya dakika 4-5. Watoto kwenye gradi zinazofuatana wanaweza shughulikia tu dakika 10 tu kama zinafurahisha.



Watoto kwenye gradi ya 6 wamepita gradi ya watoto wanaweza shughulikia dakika 15 tu za kusikiza. Somo zilizoko na vitu ndani na mawazo huvutia sana kudumisha na kudhibiti wakati wa somo la kusjiza na wanafunzi wengine wazee kiasi.

## 7. Panga muundo ule ambao wanafunzi watasoma.

Watoto wengine wameindwa na mungu kuwa wasomi wa kuona kuliko kuskiza kwa hivyo somo la kusikiza halitamwathiri kama la kutazama. Wanafunzi wengine lazima watembeze miili yao kwa hivyo kusikiza na kuona huwa haiwaathiri sana. Utafiti umeonyesha yakuwa masomo ambayo yana husisha kutembeza miili huwa yanakumbukwa na darasa nzima.. inachukua muda kutengeneza vifaa vya kuona, tengeneza hadithi vizuri, na upange kwa uhusisho wa wanafunzi. Walimu ambao wanaweka muda wana uongozi wa darasa mwema.

# Kuwa na sheria kunapunguza shida.

Kuwa na sheria kunapunguza shida.
Watoto huwa wanajuwa kile kinatarajiwa? Sheria za darasa ni rahisi na zinaeleweka? Sheria hizi huwa zina pitiwa kila wiki?

## 1. Watoto huhisi aje kuhusu sheria?

Watoto wengi wanapenda kuwa "wazuri" na wafurahishe walimu wao. Kama wanajuwa kile ambacho wanahitajika, watoto wengi watajaribu kufikia matarajio hayo. Watoto wanahisi wakiwa wamekasirika wakati wanazibwa macho na sheria zilizoundwa. Wanakuwa na aibu mbele ya marafiki wao wakati wanaelekewa na mwalimu kwa sababu ya tabia mbaya. Kwa kawaida majibu yao yatukuwa ya uasi. Watapanga kitu ili waweze kuadhibu mwalimu wao kwa kuwachezea na sheria na kuwaibisha. Hii inaweza epukwa na kuzuia. Tengeneza sheria 5 ama 6 ambazo zitatekelezwa, zifunzwe na umakini, na wafanye zoezi ili kila mtu aelewe matarajio kwenye darasa.

## 2. Kwa nini watoto huvunja sheria? Jinsi ya kuzuia.

Wakati mwingine watoto wanahitaji uangalifu ziada kuliko ule ambao wanapata na watavunja sheria ili wapate uangalifu. Kuzuia hii ni kupanga jinsi ya kupee aina ya mtoto huo uangalifu chanya(positive). Usifanye watoto wakuwe wanaomba uangalifu hadi wako tayari kuvunja sheria ili wapate. Kama mtoto yeyote wa jinsia yeyote amevunja amri, kuwa mwangalifu asipate uangalifu aliokuwa akitaka kutoka kwa kuvunja amri. Usifanye kuwe na tukio kubwa. Hakikisha watoto wanapata uangalifu mzuri zaidi kama "msaidizi" wako badala ya kusababisha shida na tukio litafanyika mara moja ama mbili na haitakuja tena. Jiulize, ni nini anataka haipatikani? Jibu linaweza kuwa tu kutembea. (ADHD) inaweza kuwa kuwa kudhibiti tu kidogo. Inaweza kuwa ni uangalizi tu mdogo. Mtoto anapata kitu ambacho kinahitajika kutoka kwa tabia mbaya. Mwalimu anahitaji kugundua ni nini na aipeane kwa njia nzuri zaidi.

### Sheria za darasa

TENDA WENGINE KWA WEMA

Tenda wengine kwa heshima

Ruhusu mwalimu wangu afundishe

RUHUSU WENGINE KUFUNDISHWA

Kuheshimu vifaa

Kuwajibika kwa vitendo vyangu

Kuwajibika kwa mafunzo yangu

## 3. Funza sheria

Kuwa na raha kuigiza tukio pale ambapo mtu anavunja sheria, hadi kwa njia ndogo, na tukio linguine pale ambapo mtoto anafuata sheria. Kuwa na uhakika kufunza tofauti katii ya wao na sheria mabayo inatarajiwa. Kwa mfano, "usitumie mikono yako kufanya kitu mbaya" inaweza vunjwa kwa kusukuma mtoto chini kwenye ardhi ama kwa kudona kiasi kwenye mkono wake ama kujaribu kuchukua penseli ya kuchora ambayo anatumia. Funza tofauti kati ya miguzo mizuri na mibaya. Kutakuwa na wakati wakushika mikono darasani na kuomba. Kutakuwa na masaa ya kukumbatiana kama kuna rafiki anahitaji kufarijiwa.

Mfano mwingine wa kufurahisha ni kufunza sheria kuhusu "kuchukua nafasi kuongea" ni kuchukua mashindano kuona ni timu ipi ya wanafunzi inaweza nyamazisha ingine kwa muda mrefu. Hii ina wakilisha atakama ni ngumu kunyamaza, haiwezekano kwa mtu yeyote kwenye chumba.



## 4. Pitia sheria zote kutoka mwanzo wa masaa yote ya darasa.

Hii ndio hatua muhimu ambayo inasababisha sheria zako zikuwe za kawaida kwa wanafunzi. Baada ya kutumia muda mwingi wa kufunza kwenye siku za kwanza mbili, pitia haraka kila wakati una darasa. Unda ratiba ambayo watoto wanatarajia wakati darasa inaanza. Kwa mfano, karibisha mwanafunzi yeyote mpya ambaye uko naye darasani, anza na ombi(fupi, ukiuliza mungu kufanya muda mabao mko nao mdogo pamoja uwe wa maana na usababishe mabadiliko mazuri kwa kila maisha inayowakilishwa.)kisha wafanye watoto waseme amri, mbona tuko nazo, an waeleze kama inahitajika(kwa mfano kuna mwanafunzi mpya)

## 5. Ambia wanafunzi ratiba na mipango

Ifuatayo, ambia wanafunzi ratiba ya hiyo siku. Wacha wajue vitu gani za kuwafurahisha umewaweke. Watagundua yakuwa una usimamizi wote wa darasa na kama darasa ikifanya tabia mbaya, itakuchukua muda kiasi kutatua na kushughulikia mtoto na njia ya kupendeza, nah ii inamaanisha yakuwa hatakuwa na muda wa kupitia vitu zote za furaha ambazo ulikuwa umepanga. Kama una masaa nyuma ya ratiba yako watajuwa yakuwa unaanguka nyuma ya ratiba, na wakati wako mbele kidogo na wanaweza cheza raundi ya mchezo. Kwenye uzoefu wangu, wanafunzi walishirikiana na mimi kwenye mpango wangu, **wakangoja kwa shughuli ijayo, na wakatekeleza sheria kwa wanafunzi wengine bila mimi kuingililia.**

# Ni sheria zipi muhimu?

Sheria zinafaa kuwa zinaenda na umri.

## 1. CHATI ZA SHERIA ZA WASOMI WACHANGA NA WATOTO WADOGO

Watoto wadogo wanahitaji kuona chati kuwakumbusha kila wakati. Kwa sbabu hawawezi soma, kwa mara mingi tumia picha. Ninginiza cheti pahala itaonekana vizuri. Hawawezi kumbuka kutoka wiki hadi wiki, kwa hivyo anza kila muda wa darasa kwa kupitia sheria na kile ambacho kila picha inamaanisha.




Sheria za darasa
Kuangalia macho
Masikio ya kusikiza
Midomo iliyo nyamaza
Mikono ya kusaida
Miguu ya kutembea

## 2. CHATI ZA SHERIA ZA GRADI YA KATIKATI YA WATOTO

Ongoza mjadala kwa ajili ya watoto na wa waamue sheria zao kwenye darasa. Wanafunzi waliozeeka kidogo huwa wanafuata amri vizuri wakati hazi peanwi na mwalimu. Huwa inafanya kazi vizuri watoto wakitumia akili zao pamoja kwaa zile sheria wanataka kwa wenyewe. Kwanini? Wakati wanahisi umiliki wa sheria, wanatarajiwa kufuata na kuitekeleza. Maoni ya walio kwa umri moja huwa yana nguvu kuliko maoni ya mwalimu kwa umri wao. Kama wangeshrirkishwa na waone jinsi vile wanafunzi wengine walikuwa wanataka sheria, hawatataka kuivunja na kuleta hasira ya wanafunzi wengine.






## 3. CHATI ZA SHERIA ZA "JUNIOR HIGH" NA SHULE YA UPILI

Wakati unafikiria kuhusu sheria, watoto wa umri huu huwa wanafikiria vitu mingi sana. Ona mfano chati ya sheria kwenye kurasa hii na pale hii ilifanyika. Mwalimu aliandija kila kit ambacho kilipendekezwa na kama darasa, wakaunganisha sheria amabazo zilikuwa zinafanana na wakapata njia kugeuza zikuwe sheria moja rahisi kuliko mingi. Chati ya sheria si picha, lakini ni maneno ya watoto wenyewe. Iweke rahisi, na pamoja fanyieni kazi maneno, kuweka yakiwa mafupi, bado kila mtu anajuwa umuhimu.


**Sheria za darasa**
**Jipee heshima**
Kuwa mwaminifu, fanya bora yako,kuwa na mtazamo chanya, shiriki, jiamini we mwenyewe
**Pee wengine heshima**
Fanyeni kazi pamoja, ngoja nafasi yako,fanya kazi ukiwa umenyamaza,kuwa mkarimu, skiza, na ukae kwa kazi.
**Heshimu kanisa**
Fuata maelezo,chukua baada yako,inua mkono, na ufuate sheria.




Kwenye darasa hili
Huwa tunafanya nafasi za pili
Huwa tunasema pole
Huwa tunasamehe
Huwa tuna heshimiana
Huwa hatukatii tama
Huwa tunaweka ahadi zetu
Huwa tunapeana moyo
Huwa tunacheka mara nyingi
Sisi ni wa(belong)
Sisi ni familia.



# Panga viwango vya adhabu kwa wale wanao vunja sheria.



## 1. Ni nani wa kulaumu? Kwanza, labda ni mwalimu.



Mwalimu alianguka kwa kuzuia. Wakati uwepo wa shida ulipoanza kukua, mwalimu lazima achukue hatua haraka, na atengeneze mabadiliko. Kwa mfano: badilisha utoaji wa somo. Uliza wanafunzi kusimama na waenee nje na kuigiza sehemu ya hadithi ambayo ishaa funzwa. Kama walikuwa wamekaa pahala pamoja kwa muda mrefu, wataanza kujipee shughuli, wakati mwingine kwa njia hasi. Lazima ugunduea yakuwa hawawezi kaa chin kwa muda mrefu. Ni makosa yako yakuwa kuna shida inaanza kukua. Haraka badilisha muundo wako wa kufunza, na ufanye watoto wafanye zoezi kwa njia yeyote, na wakati ule wanafanya ivo, badilisha vile wamekaa kusongesha watoto mbali na wengine kabla wasiwasi wa wanafuzi ukwe shida.

## 2. Hewa ya darasa: usikuwe mlinzi wa jela kuhusu amri

Uspate wasiwasi kuhusu vitu ndogo. Ukamilifu ni wa yesu, na haitarajiwikutoka kwako ama kwa wanafunzi wako. Chukua tu hatua hizi za adahabu za sheria mabazo zimevunjwa ambazo zitaharibu usalama na mazingira ya kusoma ya darasa. Wacha vitu zingine zipite ju zikiwa na kichekesho kutoka kwako, kuguza mgongo wa mwanafunzi, ama kuangalia kunakosema(na macho yako tu)yakuwa hakuenda nayo lakini hauleti shida kubwa kuihusu kwa muda huu. Kuwachia neon katikati kuangalia haraka mtoto amabaye anaanza kuvunja sheria huwa inafanya waache maramoja. Kichekesho hukuja njia mrefu na kutoa wasiwasi nje ya hali ambayo ingeleta shida. Darasa nzima itacheka kwa ajili ya kichekesho. Kuwa mwangalifu kichekesho kisielekezwe kwa mtoto, lakini kwako ama kitu,sio mtu.



## 3. Hatua za adhabu

Baada ya sheria zimeelezewa na zimeeleweka, hatua za adahabu wakati sheria ianvunjwa inafaa kuelezewa kwa watoto. Hawapendi mishangao ambayo inaweza waumiza. Mwalimu anafaa kuwa thabiti kwa kuchukua hatua hizi za adahabu labad shida ikuwe kubwa sana na inaita kutoa mtoto huyo mara moja. Kwanza ni ishara

ama onyo, inayofuata ni kutembelea wanafunzi ambao wamenyamaza, inayofuata ni kupeleka kwa kiti cha muda wan je, inayofuata nikupelekwa nje ya darasa, na kitu cha mwisho ni kualika mzazi. Huku sheria zikipitiwa kwenye mwanzo wa kila darasa, adhabu pia huwa zinapitiwa.

## adhabu zetu za kuvunja amri

1. Ishara na onyo
2. Badilisha jinsi wanavyokaa
3. Kiti cha muda wan je
4. Kutolewa nje ya darasa
5. Husisha wazazi



### 1. Ishara na onyo

Wakati mwingine ishara bila kuongea huwa inakubalika na watoto kuwa kumbusho ama onyo. Watoto huwa wanashukuru onyo kabla ya adhabu. Kwa mfano: kidole kimoja kikiwa kimeunuliwa bila kuongea inamaanisha yakuwa mtu mmoja pekee anafaa kuongea kwa sababu darasa yetu huwa hatuongei maramoja sisi wote ama kuingilia kwa sababu sisi ni wa umuhimu ama tunahitaji nafasi ya kujiongelea. Sheria ni "mtu mmoja aongee kwa wakati mmoja" na wengine wamskize na wampee umakini wao wote na wamtazame na macho". Labda chati inasema, "chukueni nafasi wakati mnaongea" darasa linaweza amua kuinu amkono kunaweza fanya kazi na utaonekana kabla ya kuongea.

**wazo:** tumia mnyama aliyeshindiliwa kama kipaza sauti.

Darasa linaweza amau watatumia mpira ama mnyama aliye shindiliwa ili waweke kwenye kati mwa pale mnajadiliana. Ni mtu mmoja pekee ambaye ameshika hio kitu anaweza kuongea. Wakati amemaliza, wanaweza rudisha kwenye kati na mtoto mwingine achukue na aongee, ama wanaweza tupia kwa mwanafunzi ambaye ameinua mkono kuashiria yakuwa anawazo linguine ambalo angetaka kuongeza kwenye mazungumzo. Mtu akisahau na aingilie, mwalimu anaweza inua kidole kimoja

kuonyesha ni mtu mmoja anafaa kuongea.  Ni onyo ambalo darasa ilikubaliana itatumia.

## 2. Badilisha jinsi ya kukaa

Kama kuzuia hakujafnaya kazi, mwalimu anafaa  mpango wa kitendo ambao hautasumbua keundelea kwa somo. Ile rahisi ni kuondoa vile watu wanaketi, weka mwanafunzi karibu na mbele, weka yeye kati ya wasichana wawili, ondoa marafiki wawili na uwaweke tofauti.. nyumaye kwa hiki kitabu kuna mengi kuhusu jinsi ya kukaa.

## 3. Kiti cha muda wa nje



Wakati mwanafunzi anavunja sheria, usiwai puuza. Darasa nzima linakunagalia. Wanafunzi wanataka mpango na amani kwenye chumba. Mwanafunzi lazima akue na adhabu. Uliza mtoto atoke kwenye kikundi na akae kwenye kiti kilicho wekwa kando pale bado wanaweza skia, lakini wakae wakiwa wamenyamaza. Wanafunzi watajuwa yakuwa kiti ni adhabu amabayo inafanana na kutumwa kwa chumba cha kulala uondokee familia. Ni adhabu ndogo, watoto wadogo wanaweza kaa hapo dakika kama 2 ama 3, waliozeeka kidogo wanahisi baada ya dakika 5, lakini si zaidi. Kwenye mwisho wa muda, waalike watoke kwenye kiti waungane na vikundi vyao. Panga kuongea na mwanafunzi kibinafsi muda ukiruhusu kujua kama walielewa ile sheria walivunja. Ni kiliwafanya wavunje hio sheria ? wazo 1: pee kila mtu shughuli ili upate muda wako na mtoto. Wazo la 2: uliza mwanafunzi akae baada ya darsa wakati kila mtu ashaa enda ili muongee mkiwa nyinyi wawili.

**wazo:** wakati wa kujidaliana: mwalimu lazima asikize upande wake mtoto wa shida

Adahbu huwa inahitaji muda wa kuonyesha mapenzi  kwa mwanafunzi na kuelezea kwa nini  tabia hio ni mbaya na kupanga vile haitafanyika tena. Kama mwalimu, usikue na hasira lakini onyeshana mapenzi, kujali na usawa. Jaribu kuelewa kutoka

kwa mtazamo wa mtoto na sababu za kufanya afanye tabia mbaya. Funguka kuskiza kile ambacho wanasema badala ya kuwakemea na kujitetea. Kuwa tayari kuwa wakili wa mtoto kuhakikisha kile ambacho kili sababisha shida kisifanyike tena na mtoto anaweza hisi yakuwa unaweza kuamini na usawa na utamlinda kwa wakati ujao. Walimu wanafaa kugundua yakuwa kulipuka kwingi ni kutoka kitu kilfanyika na mwalimu hakuona. Labda mtoto alikasirishwa na mtoto mwingine.

## 4. KUTOLEWA NJE YA DARASA


kunaweza kuwa na nyakati kona ya "muda wa nje" haifanyi kazi. Mtoto anayekaa hapo bado anavurugwa na wanafunzi wengine. Njia hio ingine kwenye ngazi ya kurekebisha ni kutoa mtoto huyo kutoka kwenye chumba. Ni muhimu kuwa na mtu wakujitolea ambaye anaweza chukua mtoto huyo amuongeleshe ya kile ambacho kina msumbua. Panga na mtu wa kujitolea pale ambapo atapeleka mtoto waongee na ile ishara ambayo itakuwa. Mfano: kupigiwa simu ama kutumia ujumbe wa simu, ama mwalimu atatuma mtoto kwendew kutoka kwenye kanisa. Mtu wa kujitolea atapee mtoto nafasi ya kutoka nje ya darasa na kujiongea. Kwa kawaida baada ya dakika 15 mtoto atakuwa amechoka na atatamani kurudi kanisa kufnaya zile vitu nzuri ambazo uliambia wanafunzi mwanzo wa darasa. Hawataki kukaa na mtu wa kujitolea badala ya kucheza mixhezo,kula vitafunio, kutengeneza hila. Lakini kabla ya warudi, wanahitajiwa kuitikia yakuwa wali fanya kitu mbaya na watubu yakuwa walivunja sheria. Wanahitajika kuweka ahadi yakuwa watafuta sheria zote ili waweze kuitikiwa kwenye darasa tena.



## 5. Husisha watoto

Sehemu ya mwisho kwenye ngazi ya adhabu, kama mawazo yaliyoko hapo juu hayakutatua shida, ni kuhusisha wazazi wake. Wacha wazazi wake waje wamchukue mtoto ama kuwe na mtu wa kujitolea kusindikiza mtoto kukaa na wao. Panga kuwe na mkutano na wazazi baada ya kanisa ili uweze kuelezea kile ambacho mtoto alichofanya na kwa nini walitolewa kwenye darasa na upate maoni kutoka kwa wazazi kuhusu kile huwafanyia kazi. Elezea kwa nini mtoto alifanya tabia mbaya jinsi watavyo elewa. Kwa mara mingi zile shida hukuwa shule ni hizo pia hukua nyumbani. Kama mwalimu na wazazi wamekubaliana jinsi ya kufanya, na wamekubaliana umuhimu wa kuhudhuria kanisa na kusoma zaidi kuhusu mungu, vitu vitaenda sawa kwenye muda ujao. Ashiria yakuwa mwanafunzi amekaribishwa kwa darasa na yakuwa huwa mnajali na mnataka asome kuhusu mungu na asiwai hisi nikama wamekatiliwa na kanisa. Kubaliana na mwanafunzi yakuwa hii ni tukio moja na ishaa pita na tutanza upya wiki ijayo.





Hatua ya mwisho: Mwanafunzi lazima aketi pamoja na familia yake kanisani.

# tumia sauti yako kudhibiti darasa lako

Toni lako la sauti ni kifaa kikubwa kwa kudhibiti darasa.

## 1. TAMBO NI MUHIMU,NONG'ONA



kwanza usiwai piga kelele kwa sauti kubwa kwa mwanafuzi. Kama mwanafunzi anahitaji onyo, nong'ona kwenye masikio ya mtoto huyo. Si biashara ya mtu mwingine, na inaweza aibisha mtoto kamainaweza semwa mbele ya darasa. Kumbuka ya kuwa heshima ya rika ni ya umuhimu juu ya gradi ya 3 kuliko kufurahisha mwalimu.

## 2. PUNGUZA SAUTI NA UULIZE JIBU KUTOKA KWA DARASA.

Kama darasa inaanza kuwa na makelele mingi wakati wa shughuli ya usanaa, tumia sauti yako kudhibiti. Angusha sauti yako hadi ikuwe laini na uulize darasa kuinua mkono kama wanakusikia. Wakati wanaopiga kelele wakiona darasa ikikujibu, tama ya kujua itawafanya wanyamaze wakijaribu kugundua kile ambacho wamekosa kusikiza. "nipee tabasamu kama unanisikia" saa zingine huwa inafanya kazi. Nimekuwa wakunyamazisha watu kwa kusema "guza pua yako kama umesikia kile ambacho nimesema".

## 3. IMBA MAELEZO




Nimeona majibu makuu wakati mwalimu anapiga makofi na anaanza kuimba na maelezo yanayofuata, watoto wote walishangaa yakuwa mtu mzima anaimba maelezo na darasa nzima ina nyamaza. Wanaskiza kwa umakini maelezo ambayo mwalimu anapeana.

# tafuta ishara ya kushika umakini wao ambao utakufanyia kazi

## 1. Ishara ya maneno yaliyosemwa

Nikiwa na wanafunzi wangu wachanga niliona ilinifanyia kazi vizuri kusema, "macho kwangu". Niliwafunza yakuwa wakati wanasikia yakuwa nimesema hivo, jibu lao mara hio ni kuacha kuongea na kuweka mikono yao kwenye mapaja na kugeuka na kuniangalia, na kusikiza kwa umakini. Tulipiga zoezi hadi wakawa wamejuwa na tukafanya zoezi ingine baadae wakati jibu yao haikuwa kama nilivyo tarajia. Ilifanya kazi kama filimbi ya refa ya kusimamisha mchezo. Nilipendelea ishara hii kwa sababu nilikuwa nayo kila wakati, kwenye barabara, kiwanja,na pahala popote na pale ambapo nlienda na darasa.

## 2. Ishara ya masikio ya sungura

Kunyamazisha kikundi, inua mkono juu ukiwa umeweka vidole mbili. Hii ina ashiria masikio ya sungura kwenye mkao wa wanafunzi wadogo na ishara ya amani kwa waliozeeka kidogo. Wanajibu kwa kunyamaza na kuchukua ishara kama hio. Wakati kila mtu ako na ishara hio juu na chumba kimenyamaza, unaweka yako chini, na wanaweza pia weka yao chini, lakini wabaki wakiwa wamenyamaza wakisikiza kile ambacho unasema. Ishara yao inahitaji kufunzwa na kupewa zoezi kidogo, lakini inafanya kazi vizuri na umati mkubwa wa watoto.



## 3. Ishara ya kupiga makofi

Ishara ingine rahisi ni kupiga makofi muundo wa "shave and a haircut". Mwalimu anaianza, watoto wanageuza uso kwa mwalimu, wakipee umakini wao wote, kisha wanamaliza. Hii ni njia ya kuzuia mikono yao kutokana na kile wanafanya wakati wa kula ama ufundi. Wanahitaji kusomeshwa muundo, na nafasi ya kufunzwa mara mingi. Usijali kuhusu mwanafunzi mpya, watasoma haraka sana kwa kuangalia tu vile wengine wanafanya. Wakati Inakuwa ya kuchosha, badilisha muundo wa kupiga



makofi ili darasa ikusikize sana na ikunakiri. Anza na muundo mfupi wa kama makofi 4, kisha ongeza hadi kwa miundo kadhaa. Wanasikiza wanarudia. Wakikosea, huwa wanacheka cheka, lakini unaweza waambia yakuwa ilikwa ngumu, na urekebishe hadi kwa muundo mfupi. Lengo lako si kuaibisha mtoto ama kumfanya ahisi akiwa mdogo, lakini kupata umakini wao na kupata udhabiti wa darasa kwa tukio linalokuja kwenye ratiba yako ya siku.

## 4. Ishara ya hoo-ha

Kiongozi anaitana "hoo-ha" na wanafunzi wanajibu "hoo-ha-ha" huku wakisimama, wakizunguka, na kukaa chini tena. Hii inasaidia wao kumakinika na kuacha kile ambacho walikuwa wanafanya kuangalia kiongozi. Wakati mwingine ni raha kuafanya mara kadhaa kwa ajili ya kupiga zoezi.

## 5. Kengele na ishara ya mwangaza



Kuzima mwangaza wa darasa hushtua watoto na wanakuwa makini mara moja. Washa mwangaza haraka wakati macho yao yako kwako, peana maelezo unayotaka. Na wanafunzi waliozeeka, nlipata mafanikio ya haraka na ii. Lakini waligundua yakuwa si dharura na wakaacha kushtuka na wangendelea kuongea hata mwangaza ukiwa umezimwa na kwa hivyo haikufanya kazi. Kengele ama filimbi inaweza shtua wanafunzi wanyamaze maramoja na waangalie mwalimu. Inaweza kuwa ya umuhimu kuangalia pale ambapo sauti inafika ili usisumbue wengine wakiwa darasa ama kanisa inayo endelea karibu.

## Jinsi Darasa hudhibitiwa na kuketi?

Watoto wanaweza dhibitiwa na mazingira. Wakati watoto wako wengi sana kutakuwa na shida. Pia, kuzuia ndio kifunguu cha mafanikio

## The teacher must assign places to sit.

### 2. Kukaa na mikeka



Watoto wadogo huwa hawashtuki kukaa kwenye sakafu kwa hivyo walimu wa chekechea huwa wanatumia mikeka midogo kutengeneza viti. Pale ambapo nilifunza chekechea kwa shule ya uma, tulitumia sampuli za zulia. Karatasi zilizoko na rangi, mfuko wa plastiki, ama gazeti zingefanya kazi vizuri. Huwa inasaidia kuwa na rangi moja ya msichana na rangi nyingine ya wavulana, kama darasa ina wanafunzi wengine mpya, mikeka hio inafaa kuwa na majina ili mwalimu aweze kupanga jinsi watakavyo kaa kila wiki na kupee wanafunzi muda wa kujitafutia mkeka wa kukalia wanapo ingia darasa. Kama mikeka haikaribiani na mwalimu anaona mkono ule unataka kusumbuana. Mwalimu ako na uhuru wa kutembea katikati mwa watoto huku akifunza.

### 2. Kukaa na viti ama benchi



Watoto walio na umri mkubwa kidogo wanapenda viti kwani hawawezi kuwa na furaha wakiwa wamekaa chini kwenye sakafu. Lakini, nimetumia sakafu na mafanikio na watoto wazee kidogo kwa kuwapa nafasi ya kusimama mara kadhaa.



## 3. Kukaa na kati(tarp)


Nje, nimeweka darasa ya watoto kwenye kati ama mbili. Hawana wasiwasi wakikalia kati kwa sababu ni safi na haina wadudu, atakama wanakaa nje kwenye uchafu. Hakikisha yakuwa wanafunzi wako kabisa kwenye kati. Jifanye yakuwa hio ni mashua nan je ya kati ni bahari, imejaa papa kwa hivyo lazima wakae kabisa kwenye kati ili wakue salama.

## 4. jinsi ya kukaa

jinsi ya kukaa pia ni muhimu. Inaitwa "crisscross applesauce) ambayo inamaanisha kuvusha miguu mbele na kukalia matako yao. Nili sahihisha mtoto yeyote ambaye alikaa kama miguu yake imekunjwa, kwani inafanya kuamka kuwe rahisi na magoti, na ngumu kwa mwanafunzi aliye nyuma



kuniona. Wanaweza ingia kwa shida kutoka kwa nafasi ya miguu ilito fungwa na mwalimu anaweza ona kwa urahisi kabla ifanyike na achukue hatua. Ni muhimu kujua kufanya wanafunzi wazee kidog waamke, panga mapumziko, kuwa zuia kutembea kwa sababu wako na wasiwasi wa kimwili.



## rembesha eneo la darasa




sehemu ya kupanga mazimgira ni kupanga kile ambacho mtoto ataangalia wakati akili yake itaenda kwa sekunde kadhaa. Usikose mwongozo wa kuoekana.

Weka mabango ambayo yanaelekeza mawazo ya mtoto kwa mungu. Ninginiza mandhari ya somo ama aya ya bibilia kusaidia mtoto kuikariri.

Kama una darasa nje, ninginiza vitu na mabango kutoka kwa mti, ama nje ya ukuta wa kanisa.

Kama uko ndani  na uko na ukuta, unaweza pia ninginiza karatasi za kazi ama kazi ya usanii kuwaonyesha yakuwa unawathamini. Wangetaka kufanya bora kwa sababu haijalishi, si siri na kila mtu atakuwa anaangalia. Unaonyesha yakuwa wao ni wa umuhimu kwa mungu na kwako. Kama hakuna kitu cha kuangalia, macho yao itaangalia wanafunzi wengine kuwapee nafsi ya utundu.






## Hitimisho: ni nini muhimu sana?

Kuzuia ndio funguo la kukosa shida ambazo zinahitaji adhabu. Kuzuia huwa kunatumia mwalimu muda mwingi nyuma ya matukio lakini zawadi zinafaa.
Kuwa na sheria zinazoeleweka na rahisi ambazo zinafunzwa na kutekelezwa na adhabu

Mwalimu aliye na kudhibiti darasa vizuri huwa anangoja kufunza, anafurahia kuwa na watoto, na anaona tunda kubwa la roho kutoka kwa masomo. Utahisi furaha ya kutumiza mwito wako. "nendeni kwenye dunia yote na MFUNZE neon la mungu na mtengeneze wafuasi.." na kutimiza utumizi wa zawadi uliyopewa na mungu ya kufunza.

Darasa yako itakua kwa sababu watoto watakuwa na raha kwenye kanisa na wataalika marafiki wao kumbukumbu zao za kanisa wakati watakuwa wazima hazitakuwa chungu ama za kujuta. Mawimbi ya ushawishi yatafika mbali na upana, kizazi hadi kizazi, wakati utapeana ubora wako wote kwa kufunza.,



Wizara rasilimali Free watoto:

# Watoto ni wa muhimu

childrenareimportant.com/swahili/

*"Wewe ni hapa ili kubadilisha maisha, tuko hapa kukusaidia."*

Controlling the
Chaos
Swahili

13202

www.ChildrenAreImportant.com
info@childrenareimportant.com
01-52-592-924-9041

Follow us on: YouTube facebook